Karibia Uwe Mkristo

na

Ellis Forsman

Karibia Uwe Mkristo

na

Ellis Forsman

Januari 14, 2012

Karibia Uwe Mkristo

Matendo 26:27-29

Matendo 26:27-29, "*Mfalme Agripa, je! Wawaamini manabii? Najua ya kuw wawaamini. Agripa akamwambi Paulo kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi niwe Mkristo. Paulo akamjibu namwomba Mungu kwamba ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanao nisikia leo wawe kama mimi isipokuwa, vifungo hivi.*"

Jibu hili la Mfalme Agripa kwa Paulo kinaonyesha kuwa kuna kitu ambacho ni cha kukaribia na bado si Mkristo

Kuna wale wanaokwenda zaidi juu ya hili swala la kufanyika Mkristo.

Hebu na tuangalie kile kinachoonyeshwa kwa kuwa karibia Mkristo, na pia kinachoonyeshwa kwa kuwa Mkristo kwa ujumla.

Karibia Mkristo

Watu wengine wanafikiria kwamba wao ni Wakristo kwa sababu walizaliwa, wakalelewausoma katika taifa la Kikristo, au kwa sababu wamezoezwa katika ustarabu wa Kikristo.

Lakini watu kama hao ni Wakristo tu kwa uanisho wa kijiogorafia na si katika weledi na kujitoa.

Kwa uanisho huo, mmoja anaweza kuwa wa kimuhamedi kama akiishi katika bara la Asia, au wanaoamini katika miungu ya Shinto kama akiishi Japan, au katika miungu ya machafuko kama akiishi Uchina.

Katika swala kama hili, Carl Sagan (mtu ambaye hakumwamini Mungu) angeweza kuitwa Mkristo.

Wengine wanachukuliwa kuwa Wakristo tu kwa sababu wameamua kwa niaba ya Ukristo katika akili zao wenyewe dhidi ya dini zote.

Wanaamini dini ya Kikristo kuwa ya kipekee, na wamejiahidi wakati kwa wakati wenyewe wakiwa wagonjwa, au vinginevyo wataarifiwe, kwamba watakuwa Wakristo kwa hakika, lakini wameahiri umuhimu wote wa swala hili la kujitoa kikamilifu kwa Kristo kwa kutii injili.

Wengine wanafikiri kuwa ni Wakristo kwa sababu wamekuwa na nidhamu ya Ukristo.

Wanamsimamo wa kiaminifu.

- Wasingeweza kuiba mali za majirani zao.

- Wasingeweza kudanganya au kusema uongo, aidha tajiri au maskini.

Kwa karibu wao ni wakweli.

- Wasingeweza kushuhudia uongo.
- Wasingeweza kusema umbea au kusengenya majirani zao.

Hivi vitu "karibia" Mkristo haifanyi chochote ambacho injili inakataza.

- Hawalichukui jina la Bwana bure.
- Wanaachana na ibada ya sanamu, uzinzi, ulevi, tama, na uaji.

Kama kiongozi kijana tajiri katika Math. 19:20, wangeweza kusema kuhusu amri ya Mungu ya kweli, "

Watu kama hao Yesu angewaambia kama alivyowaambia waandishi katika Marko 12:34, "*…Hamko mbali na ufalme wa Mungu. …*"

Mkristo wa ujumla

Kuwa Mkristo kwa ujumla ni kuwa mwanafunzi wa Kristo.

Matendo 11:26, "*Hata alipokwisha kumuona akamleta Antiokia ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa kwanza Wakristo hapo Antiokia.* Kuwa mwanafunzi wa mtu ye yote ni kuwa mfuasi wa mtu huyo, na mwanafunzi wa mafundisho yake.

Kuwa mwanafunzi wa mtu anayefundisha machafuko ni kudumisha mafundisho yake.

Hivyo, kuwa mwanafunzi wa Kristo ni kujikana kwa mtu mwenyewe, kuchukua msalaba na kumfuata Yesu.

Luka 9:23, "*Akawaambia wote, ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, abebe msalaba wake na anifuate.*"

Kuwa Mkristo wa ujumla inamaanisha kuwa mshiriki wa kanisa la Kristo.

Katika kufanyika mwanafunzi wa Kristo, mtu lazima abatizwe katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

Math. 28:19, "*Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.*"

Mtu anapobatizwa, anazidishwa katika kanisa.

- Matendo 2:37-38, "*Walipoyasikia haya, wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akajibu akawaambia, tibuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Matendo 2:41, "*Wale waliolipokea neno lake kwa furaha wakabatizwa; na siku hiyo watu elfu tatu walizidishwa.*"
- Matendo 2:47, "*Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Na Mungu akalizidisha kanisa kila siku wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Kuwa Mkristo wa ujumla inaonyesha kwamba mtu amezaliwa kwa mara ya pili.

Yohana 3:3, "*Yesu akajibu akamwambia, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa mara ya pili hawezi, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*"

Bila kuelewa maana ya maneno ya Kristo, Nikodemo akamuuliza Yesu:

Yohana 3:4, "*…Awezaje kuzaliwa mtu akiwa mzima? Aweza kurudi tumboni mwa mamaye, na azaliwe?*"

Katika jibu la swali hili, Yesu akasema:

Yohana 3:5, "*Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu.*"

Lakini kuzaliwa huku kupya kuna hitimishwa vipi?

Wengine husema kuwa ni mwongozo wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu juu ya moyo wa mwenye dhambi, ambayo inaleta ushawishi na kuongoka kwake.

Kwamba ni lazima aungane na kanisa Fulani, na kwenye ubatizo wake majini anazaliwa mara ya pili ishara ya kuzaliwa kupya, ambayo ni ya maji.

Lakini hii inaweza kufanya ubatizo mara mbili, na Biblia inafundisha kwamba kuna ubatizo mmoja tu.

Waef. 4:5, "*Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja.*"

Pia, hii itafanya uzazi mbili za nyongeza; Yesu hakusema, "mtu asipozaliwa tena na tena," bali alisema, "*Mtu asipozaliwa tena*,".

Wakati neno la Mungu linahubiriwa kwa uaminifu, Roho Mtakatifu anafanya kazi, kwa sababu Yesu alisema:

Yohana 6:63, "*Roho ndiyo itiayo uzima , mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni Roho tena ni uzima.*

Waru. 10:17, "*Basi imani huja kwa kusikia na kusikia neno la Mungu.*"

Wakati imani inapopandikizwa katika moyo, hii uwaongoza watu kutaka kubatizwa, kwa maana Yesu alisema:

Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

Wakati aliyeamini anapobatizwa, anabatizwa katika Kristo.

Wagal. 3:27, "*Kwa maana wengi wenu mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Paulo alisema katika 2 Wakor. 5:17, "*Mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yote yamepita tazama yamekuwa mapya.*"

Hivyo, kuwa kiumbe kipya ni kuliwa tena.

Kuwa Mkristo wa ujumla ni kuolewa kwa Kristo.

- Waef. 5:25-32, "*Enyi waume wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa akajitoa kwa ajili yake. Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa utukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo, bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna mtu auchukiaye mwili wake popote, bali huulisha na kuutunza kama Kristo naye alivyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo wa mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.*"

- 2 Wakor. 11:2, "*Maana nawaonea wivu, wuvu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja ili nimlete Kristo bikira safi."*

- Waef. 5:24, "*Hivyo kama jinsi kanisa limutiivyo Kristo, vivyo hivyo wanawake nao wawatii waume zao katika mambo yote.*"

Musa aliwaamuru Waisraeli katika Kutoka 20:8, "*Uikumbuke Sabato na kuitakasa.*" Lakini kanisa halipaswi kupata muongozo wake kutoka kwa Musa, bali kwa Kristo.

Daudi alisema kwa Israeli katika Zaburi 33:2, "*Mshukuruni BWANA kwa kinubi, kwa kinanda cha nyuzi kumi, mwimbieni sifa.*"

Lakini kanisa halipo katika ushirika wa Daudi, bali Kristo.

Wakol. 3:16-17, "*Neno la Kristo na likae kwa wingi mioyoni mwenu katika hekima yote; mkifundisha na kuonyana katika zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, mkiimba kwa neema mioyoni mwenu kwa Bwana. Na*

lolote mfanyalo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu na Baba kwa yeye."

Tofauti, na kile Daudi alichomwambia Israeli kufanya haikuwa na baraka kutoka kwa Mungu.

Amos 6:1,5, "*Ole wao wanaostarehe katika Sayuni, na hao wanaokaa salama katika mlima wa Samaria, watu mashuhuri wa taifa lililo la kwanza, ambao nyumba ya Israeli huwaendea. Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda na kujifanyizia vinanda vya namna nyingi, kama vile Daudi.*"

Kwa nini tunapaswa kuwa Mkristo na Mkristo pekee

Kwa sababu jina "Mkristo" ni jina ambalo Mungu ametoa.

Kume kuwa na watu katika ulimwengu ambao wanaeleza kwamba jina "Mkristo" ilitolewa kwa kuholewa na maadui wa Kristo kwa wafuasi wake.

Wanafunzi Wakristo wamekuwa wakishindana juu ya swala hili ambalo ni la uongo kwa miaka. Ni sawa na uongo uliosemwa na mtu mmoja na kutapakaa kote kwa neno la mdomo ambao haufi.

Chanzo chake hakiwezi kupatikana popote katika maandiko au historia. Kwa hakika hakuna uthibitisho wa kuweza kutetea wazo hili.

Zaidi sana, kama jina "Mkristo" lilitolewa kutoka kwa imani na maadui wa injili, je! Chochote ambacho kimekuwa cha milele, "*jina mpya"* ambayo mdomo wa Mungu iliita juu ya watoto wake?

- Isa. 62:2, "*Na mataifa wataiona haki yako, na wafalme wote watauona utukufu wako, nawe utaitwa jina jipya, litakalotajwa na kinywa cha BWANA.*"
- Isa. 65:15, "*Nanyi mtaliacha jina lenu kuwa laana kwa wateule wangu. Na Bwana MUNGU atakuua; naye atawaita watumishi wake kwa jina linguine.*"

Mungu aliahidi kwamba yeye, mwenyewe, angewapa watu wake majina mapya. Aliahidi kwamba angeweza kutoa kwa wakati ambapo "*Mataifa na wafalme*" wameona haki yake.

Haikuwa jina ambalo maadui wangeweza kutoa.

Isa. 56:5, "*Nitawapa hawa nyumbani mwangu, na ndani ya kuta zangu kumbukumbu na jina lililo jema kuliko kuwa na wana wa binti; nitawapa jina lidumulo milele lisilokatiliwa mbali.*"

Isingekuwa jina ambalo lingeibuka zaidi ya ushirika wa watu wa Mungu. Ilitolewa katika nyumba yake na ndani ya kuta zake.

Matendo 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na Kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.*"

Hii ilitokea katika kifungu kimoja cha kitabu cha Matendo baada ya kuongoka kwa Kornelio na nyumba yake, ambao walikuwa ni mataifa, ikitimiza unabii katika Isaya kwamba mataifa watauona haki yake, na ya kwamba wataitwa kwa jina mpya.

1 Petr. 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya , bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"

Petro alitambua jina hili kwa wafuasi wa Kristo.

Matendo 26:28, "*Agripa akamwambia Paulo, kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo.*

Jina hili lilitambulishwa mbele ya wafalme, kama jinsi Mungu alivyosema ingetokea nyuma katika kitabu cha Isaya.

Kwa nini uwe Mkristo na Mkristo pekee? Kwa sababu jina Mkristo ni jina tunalomtukuza nalo Mungu.

Wakati mwingi uliopita, chini ya Agano la Kiyahudi, Mungu alikuwa na jina kwa watu wake kuweza kuvaa, na jina hilo lilikuwa ni Israeli.

Kwa nini? Kwa sababu jina "El" ili kuwa ni jina la Kiyunani iliyomaanisha "Jehova", hivyo kila wakatika jina la "Israeli" ilipoongelewa, jina la Mungu lili heshimiwa.

Kuna majina mengi ya Makristo leo wingi, na katika idadi gani ya hayo majina tunayoweza kumtukuza Mungu?

1 Petr. 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"

Hitimisho

Je wewe ni Mkristo? Si karibu, bali kwa ujumla?

Kumbuka, unaweza kuwa karibu kuokolewa na ukapotea.

Unaweza kulipia kwa miaka katika mji na iwe karibu kulipiwa, na pia ukaikosa.

Karibia unaweza ukawa vizuri, na ukafa.

Kuna watu wengi "karibia", lakini si kwa ujumla washawishike kuwa Wakristo. Kuna wakina Agipa wengi katika ulimwengu.

Kama wewe si Mkristo, Kristo hana sehemu katika maisha yako.

Math. 12:30, "*Mtu asiye pamoja nami yu kinyume change, na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya.*"

Kama wewe si Mkristo wa ujumla , basi mwamini Bwana Yesu kw moyo wako wote.

Na utubu dhambi zako.

Na katika kukiri kwako mbele za watu jina la Yesu.

Ubatizwe katika Kristo na hapo uwe Mkristo kamili. Uishi kwa uhuru kwa hilo jina maisha yote, alafu upokee zawadi ya Mkristo kati utamu tena na tena.